

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



Unapojibutafadhalitaja:

HM/SI/M.40/81VOL. IV/43

09 January, 2024

TANGAZO

KWA UMMA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA KUHUSU KUFUNGULIWA KWA UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1) ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida anatangaza kufunguliwa kwa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu ambapo jumla ya shilling **999,804,957** zimetengwa katika robo ya 3 ya mwaka wa fedha **2024/2025**

Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia ya mfumo katika Ofisi za serikali za Mitaa (Kijiji/Kata) zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kwa njia ya mfumo wa kieletroniki.
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za Ujasiriamali.
- (iii) Kikundi cha W



Edit with WPS Office

ake, na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi

kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 7 a(1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kieletroniki (tembelea tovuti: **mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambalisho vifuatavyo; Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa kijiji/mtaa kwa kuandika jina lake, saina na kugonga mhuri wa serikali ya Kijiji, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo wa kieletroniki na taarifa ya akaunti ya benki yenye jina la kikundi au Jina la mtu mwenye ulemavu mmoja aliyekosa wenzake wa kuungana nao

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 8 mwezi 2 mwaka 2025

Tangazo hili limetolewa na: -



MBOYA E. W
**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA
SINGIDA.**

**MKURUGENZI WA MANISPA
SINGIDA**



Edit with WPS Office